TANGAZO LA SERIKALI NA. 236 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA ISELAMAGAZI YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Iselamagazi ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina kwa eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

*Tangazo la Serikali Na. 236 (Linaendelea.)*

______

JEDWALI

______

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 512606.317MS, 9610905.535KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KS85º02'56.28''MS kwa umbali wa kilomita 3.421 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 516028.265MS, 9610609.100KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki - Kusini katika uelekeo wa KS67º04'50.55''MS kwa umbali wa kilomita 1.74 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 562630.40MS, 9606160.48KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS05º34'25.24''MG kwa umbali wa kilomita 2.86 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 517356.319MS, 9607084.036KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KZ89º50'03.13''MG kwa umbali wa kilomita 3.65 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 513706.622MS, 9607094.597KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ03º38'05.30''MG kwa umbali wa kilomita 2.53 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 513546.107MS, 9609621.415KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi - Kaskazini katika uelekeo wa KS76º38'45.61''MS kwa umbali wa kilomita 1.38 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G yenye majira - nukta 513546.107MS, 9609621.415KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ23º01'43.67''MS kwa umbali wa kilomita 1.032 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*